

SHULE YA UPILI YA GATITU S.L.P. 01030 ,327 GATUNDU  
KIDATO CHA KWANZA  
MUHULA WA TATU, ( 2014)

JINA.....NAMBARI.....

***soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata***

1. Dunia kitu dhaifu, si ya mtu kunyetea,  
Usione ufanifu, na furaha kila njia,  
Kumbuka na uvunjifu, kama ndwele hukujia,  
Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.
2. Anasa usiandame, kwa pupa kuzipapia,  
Heri moyo fanye tume, uche na kuzikimbia,  
Hakuna mume wa dume, na wala hatatokea,  
Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.
3. Wako wapi mashujaa, wenye nguvu kila njia,  
Ziliwafika nazaa, wakabaki kujutia,  
Ndunia ina hadaa, yataka kuzingatia,  
Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

**maswali**

- i)Taja vina vyote vya utao katika ubeti wa pili ( alama2)  
.....  
.....  
.....
- ii)Taja kibwagizo cha ushairi huu (alama 1)  
.....
- iii)Taja mleo wa ubeti wa tatu ( alama1)  
.....
- iv)Eleza mpangilio wa mizani katika ubeti wa kwanza ( alama 2)  
.....  
.....  
.....

v) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu za kutetea jibu lako

(alama 3)

.....  
.....  
.....

vi) Kwa nini shairi hili ni la kiarudhi

(alama 2)

.....  
.....

vii) Taja jambo moja ambalo mshairi anaeleza liepukwe

(alama 1)

.....

vii) Andika maneno haya kwa lugha ya kawaida:

(Alama 1)

Ndu:.....

Uche:.....

2. a) Majina yafuatayo yamo katika ngeli gani?

(alama 2)

Mwigo.....

Ujinga.....

Sifa.....

Wadhifa.....

b). Tumia alama zifuatazo kikamilifu katika sentensi.

(alama 2)

i) koloni:.....

.....

ii) alama ya hisi:.....

c) Andika sentensi hii katika hali ya udogo.

(alama 2)

Mwizi huyu atasalitiwa na mtoto wake.

.....

d) Tunga sentensi kuonyesha tofauti za kimaana kati ya vitate hivi. (alama 2)

chaka:.....

shaka:.....

e) Bainisha aina za maneno katika sentensi hii: (Alama 3)

Wachache walisimama nje ya ukumbi ule jana.

.....

f) Toa mifano ya maneno yenye muundo wa: (Alama 3)

i) silabi funge:.....

ii) mwambatano wa konsonanti mbili na irabu:.....

iii) irabu pekee:.....

g) i. Onyesha sehemu mbili za methali ifuatayo: (Alama 2)

**Mwangata mbili moja humponyoka:**

.....

ii) Taja methali nyingine iliyo na maana sawa na: **Chovya chovya humaliza buyu la asali:**

.....